**Andaa kuni za kutosha**

**Ukaushaji**

- Mabadiliko yafuatayo hujitokeza wakati wa ukaushaji wa majani ya tumbaku unapofanyika
- Kupotea kwa rangi ya kijani na kujitokeza rangi ya njano
- Kubadilika kwa wanga na kuwa sukari
- Kupungua kwa kiwango cha maji kwenye jani
- Kusimamisha shughuli za vimeng'enyuo (enzymes) ambavyo ni vichocheo vya mabadiliko ya kikemikali

Hatua za ukaushaji

- Kuna hatua nne ambazo tumbaku hupitia wakati wa ukaushaji
- Kubadili rangi ya jani kutoka kijani kuwa njano
- Hatua hii hutelekezwa kuanzia nyuzi 90 za F na kukamilika katika nyuzi 100 za F na huchukua wastani wa masaa 30 hadi 60 (siku 2-3) kutegemea uzito wa jani, hali ya hewa na sehemu jani lilipovunwa kwenye mmea.

Mambo ya kuzingatiwa

- Anzisha mvuke ndani mara baada ya kujaza tumbaku kwenye bani
- Tandaza magunia yaliyolowanishwa maji juu ya bomba za mvuke
- Anzisha mvuke endapo fukuto lililopo kwenye bani halitoshelezi
- Funga madirisha yote juu na chini kuhifahdi fukuto hadi tumbaku itakapokuwa imegeuka rangi na kuwa njano
- Kuimarisha rangi
- Kazi hii hufanyika kuanzia joto la nyuzi 105 za F na kukamilika joto linapofika nyuzi 125 (siku moja)
- Mambo ya kuzingatiwa

Ondoa magunia yote uliyo kuwa unamaanisha

- mvuke/fukuto kwenye bani
- Fungua madirisha yote ya chini na yale ya juu
- yafunguliwe nusu huku ukipadisha joto kiwango cha nyuzi 2 za F kwa saa
- Joto likifika nyuzi 110 za F libakizwe katika kiwango hicho kwa kiasi cha saa sita hivi.
- Pandisha joto kutoka nyuzi 110 hadi 125 kwa kiwango cha nyuzi 1 hadi 2 za F kwa saa na
- Epuka kupandisha joto kwa haraka zaidi kwa vile utafikisha nyuzi 125 za F wakati majani bado yana maji mengi hali ambayo hufanya tumbaku kuwa na rangi ya kahawia na kushuka ubora
- Epuka kupandisha joto polepole sana kwa vile kufanya hivyo huozesha tumbaku
- Kukausha majani
- Pandisha joto taratibu kwa wastani wa nyuzi 2 hadi 3 kwa saa taratibu kwa hadi nyuzi 140 za F
- Katika hatua hii madirisha yote ya chini yanafungwa wakati yale ya juu yanafungwa robo tatu tu
- Kukausha migongo
- Pandisha joto kuanzia nyuzi 140 F hadi 160 katika kipindi cha kati ya saa 20 hadi 32 kutegemea uzito wa majani
- Madirisha yote yawe yamefungwa
- Kuhakikisha kama tumbaku imekauka vunja mgon-go wa jani na ukikatika kwa urahisi ni dalili kuwa tumbaku imekauka
- Baada ya kuhakikisha kuwa tumbaku imekauka zima moto kabisa, fungua milango na madirisha ili tumbaku iweze kupoa

KWA MAWASILIANO :

TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU

TANZANIA (TORITA)

S.L.P 431,

TABORA.

Barua pepe : info@torita.or.tz

Tovuti:*www.torita.or..tz*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA

TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU TANZANIA (TORITA)



# *Njia sahihi ya uzalishaji tumbaku shambani*

**Uwekaji dawa ya kuzuia vikonyo**

- Mara baada ya kuzuia vitumba vya maua weka mchanganyiko wa dawa ya maotoea na maji
- Hakikisha dawa haikumwagikii kwenye ngozi na pia kwenye jani
- Iwekwe sehemu ilipokatwa kitumba tu
- Mkulima anashauriwa kuvaa gloves kwa ajili ya kujikinga na dawa isimwagikie kwenye mikono

**Mmea uliokatwa kitumba cha maua**



| Aina ya dawa | Dozi | Jinsi ya kuweka | Kuzuia |
|---|---|---|---|
| Yamaotea super (Flumentralin+Butralin) | Lita moja kwa hekta | Changanya mililita 8 za yamaotea katika lita moja ya maji (mililita 80 za yamaotea katika lita 10 za maji) | Vikonyo |

*Jinsi ya kuweka dawa ya vikonyo*

**Njia za uwekaji**

- Njia inayopendekezwa ni kutumia hand applied cups njia inayofuata ni squeegee bottle
- Njia ya tatu ni knapsack application

**Kuvuna tumbaku**

- Mambo muhimu ya kuzingatia

◊ Jaribu bani/mabani yako siku chache kabla ya kuanza kuvuna tumbaku ili kuhakikisha kama yanafanya kazi.

◊ Vuna tumbaku asubuhi kuanzia saa mbili hadi saa tano kwa siku zenye jua kali. Majani yanayovunwa wakati wa jua kali hunyauka na kuwa matatizo katika kubadili rangi .

◊ Majani yaliyovunwa yahifadhiwe kivulini yasinyauke wakati yanasuburi kusukwa kwenye mianzi

◊ Zuia michubuko kwenye majani ya tumbaku sehemu yenye michubuko haibadili rangi wkati wa ukaushaji, hubaki kijani hadi mwisho

◊ Tumbaku iliyovunwa isukwe kwenye mianzi, ipangwe kwenye bani na kuanzisha mvuke siku hiyo hiyo ilipovunwa. Ukichelewesha ubora wake hupungua

◊ Hakikisha unavuna majani yaliyokomaa. Kwa uvunaji wa kawaida vuna majani mawili kwa mmea katika kila mchumo

◊ Unaweza kuvuna mara moja kwa wiki hadi mara mbili kutegemeana na hali ya uivaji wa aina ile ya tumbaku.

◊ Majani yanayowiana kiuvunaji au ukomavu yawekwe pamoja

◊ Uchumaji wa majani huanza sehemu ya chini mmea wa tumbaku kwenda juu.

**Dalili za kukomaa kwa jani la tumbaku**

- Kubadilika kwa rangi ya jani kutoka kijani kibichi kwenda kijani chepesi
- Ikumbukwe kwamba ukame, upungufu wa rutuba au mbolea na kuzidi kwa mvua pia kunaweza kusababisha badiliko hili la rangi
- Ncha ya jani hubadilika rangi na kuwa njano na jani lenyewe huinama. Kadhalika pembezoni mwa jani huwepo rangi ya kijani chepesi kinachokaribiana kuwa njano
- Jani linapokomaa mafuta hupungua
- Vinyweleo vyeupe ambavyo huwepo zaidi upande wa chini wa jani hupungua sana au kutoweka kabisa
- Kuwa na vidoadoa vyeupe vya ukomavu. Dalili hujionyesha kwa wazi zaidi katika majani ya sehemu ya katikati ya shina la tumbaku.
- Mgongo wa jani unakuwa mweupe zaidi ya ule wa jani ambalo alijakomaa na una tabia ya kukatika kwa urahisi zaidi

**Mambo muhimu ya kuzingatia kwenye usukaji wa tumbaku**

- Tumia mianzi yenye urefu wa sentimita 140
- Suka majani kwenye mianzi ukiacha sentimita 10 kila upande wa mwanzi
- Nafasi zilizoachwa ndizo zitakazokalia reki ya bani
- Suka majani kufuatana na ukubwa/udogo. Uivaji/ukomavu kila yanayofanana yawe pamoja katika mwanzi
- Suka vitita vya majani mawili hadi matatu. Kitita kimoja na kingine vielekeane migongo
- Nafasi kati ya kitita kimoja hadi kingine ni sentimita mbili nanusu hadi tano
- Suka majani kwa kutumia nyuzi za jute (jute twine)

**Upangaji wa tumbaku kwenye bani**

- Mianzi yenye majani ambayo kwa bahati mbaya yamevunwa yakiwa machanga ipangwe kwenye reki za juu kabisa kwenye bani halafu ifuatiwe na majani yaliyokomaa itakiwavyo
- Mianzi iliyoiva kupita kiasi ipangwe katika reki za kwanza kutoka chini
- Ni muhimu kuzingatia ujazo sahihi wa tumbaku
- Kujaza tumbaku zaidi ya uwezo wa bani husababisha tumbaku kuoza
- Nafasi ya kutoka mwanzi mmoja hadi mwingie juu ya reki iwe sentimita 15

**Ukaushaji wa tumbaku**

- Mambo ya kutekeleza kabla ya kuanza kukausha tumbaku
- Chombo chenye maji kiwe karibu na mlango wa bani
- Viwepo vipande vya magunia vitakavyo loweshwa na maji na kutandazwa kwenye mabomba ilil kuanzisha mvuke kwenye bani .
- Tundika kipima joto kwenye bani sehemu ya katikati. Epuka kutunduka kipima joto karibu na bomba na mwanzo kutoka kwenye jiko au karibu sana na mlango kwani kipimo

Kitaonyesha joto la juu sana au chini sana kuliko hali halisi iliyomo katika bani zima